

ULINZI WA AINA ZA MMEA/MBEGU NA AINA ZINAZOLINDWA NI NINI?

Ulinzi wa Aina za Mmea (PVP) ni ulinzi wa kisheria anaopewa mzalishaji wa mmea/mbegu aliyegundua na kutengeneza aina mpya ya mmea/mbegu. Ulinzi huu hutolewa kwa kumpa haki mzalishaji ya kumiliki aina hiyo ya mmea na kudai malipo (mrabaha) kutoka kwa yeyote anayetaka kuitumia. Haki hii iliyotolewa kwa mzalishaji huitwa 'Haki ya Mzalishaji wa Mmea'. Aina mpya ya mmea ni kama, kwa mfano, mbegu chotara ya mahindi. Pia inajulikana kama "aina inayolindwa."

Haki ya Mzalishaji wa Mmea pia inahusu aina yoyote ya mbegu iliyohifadhiwa kutokana na mavuno ya aina hiyo ya mbegu iliyolindwa. Hii ina maana kwamba wakulima hawaruhusiwi kubadilishana, kushirikiana au kuuziana aina yoyote ya mbegu iliyohifadhiwa kutokana na aina inayolindwa bila ya kulipa mrabaha kwa mzalishaji wa mmea. Mbegu mpya itabidi zinunuliwe kwa kila msimu wa kupanda.

Hata hivyo mbegu ambayo mzalishaji 'amegundua' na 'kuiendeleza' imetoka kwenye mashamba ya wakulima hawa. Kwa hiyo, Haki ya Mzalishaji wa Mmea zinakinzana na Haki za Wakulima.



Iwapo itawalazimu wakulima kununua mbegu mpya kwa kila msimu wa kupanda, hii itawafanya wakulima kuwa tegemezi na kupoteza uhuru wao na uanuwai ya mbegu. Hawatakuwa tena wazalishaji wa mbegu, bali watakuwa ni watumiaji tu wa mbegu iliyotayarishwa na wazalishaji na kuuzwa kwao na makampuni ya mbegu.

